HATARI NA HASARA ZA KURUDI NYUMA NA KUACHA WOKOVU.

Jiangalieni nafsi zenu msiyapoteze mliyoyatenda, bali mpokee thawabu timilifu.

(2Yohana 1:8)

Na

GILBERT RUWAICHI MAMBALI.

Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo;tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo,haki ile itokayo kwa Mungu,kwa imani; (Wafilipi 3:8-9)

Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake,wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake;bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii,ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana,nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana,(Yeremia 9:23-24)

YALIYOMO.

Utangulizi

SURA YA KWANZA

Nini kinatokea mtu anapo okoka.

SURA YA PILI.

Sababu za waamini kurudi nyuma na kuacha wakovu.

SURA YA TATU.

Dalili za kurudi nyuma na kuacha wokovu.

SURA YA NNE.

Hatari na hasara za kurudi nyuma na kuacha wokovu.

SURA YA TANO.

Ikiwa umerudi nyuma au umeacha kabisa wokovu.

SURA YA SITA

Ikiwa umesimama imara kwenye imani ya wokovu.

SURA YA SABA.

Ikiwa bado hujamwamini Yesu.

UTANGULIZI.

Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. (Warumi 10:9-10)

Nimeandika kitabu hiki maalum kwa watu wanne wa muhimu sana mbele za Mungu,wewe ukiwa ni mmojawapo.

Mtu wa kwanza niliyemwandikia ujumbe wa kitabu hiki ni yule ambaye amerudi nyuma na ameacha kabisa wokovu.Ingekuwa tunajadili mambo ya mpira wa miguu kundi hili ningelipa jina la kundi la kifo, lakini hapa nimeliita kundi la *hatari;* kundi linalohitaji kufanya maamuzi ya haraka. Huyu ni yule ambaye kama wokovu ingekuwa ni kundi la whatsapp basi ningetumia yale maneno ambayo huwa tunayatumia kuwa ame left group kwa maana ya kwamba amejiondoa kwenye kundi la watu walioamini.Tutajadili kwa undani kwenye sura zitakazofuata,lengo la kitabu hiki ni kumkumbusha mtu huyu hasara anazozipata na hatari zinazomkabili mbele yake kwa hatua aliyonayo sasa ili akumbuke wito wa Yesu msalabani na kurudi kwenye mstari wa imani, kwa sababu mpaka anasoma kitabu hiki bado anayo nafasi.

Mtu wa pili niliyemuandikia ujumbe huu ni mtu ambaye amepoa,mwandishi wa kitabu cha ufunuo anawaita siyo moto na wala siyo baridi, na hata yeye mwenyewe hajui kama bado yupo kundini au alishatoka. Hana uhakika endapo Yesu atarudi leo au endapo ataondoka leo duniani atakuwa kwenye kundi gani kati ya makundi mawili ya umilele, kwa sababu sote tunajua kuwa hakuna kubahatisha ni mawili aidha milele pamoja na Bwana au jehanamu ya moto. Kitabu hiki kina ujumbe na maarifa ya awali ya kumkumbusha na kumsaidia kurudi kwenye maisha ya uhakika juu ya wokovu. Hii ni kwa sababu zipo hatari na hasara endapo mtu huyu ataendelea kuishi maisha ya wokovu uliopoa na usio na uhakika wa leo na kesho.

Mtu wa tatu niliyemuandikia ujumbe wa kitabu hiki ni yule ambaye ana uhakika na wokovu,pamoja na mambo mengine yote, Yesu ni Bwana na mwokozi wa maisha yake. Kitabu hiki kina sura ambazo zitamkumbusha namna ya kukomaa na kuendelea kutunza imani mpaka mwisho, kwa sababu kama unavyofahamu mwisho mwema ni bora kuliko mwanzo mwema. Pamoja na kuanza vizuri bado una jukumu, hatua na

wajibu wa kupambana mpaka mwisho ili kuhakikisha unamaliza vizuri. Usiwe kwenye lile kundi ambalo biblia imewatambua kuwa walianza vizuri lakini wakamaliza vibaya;Walikuwepo lakini sasa hawapo tena, hata shuhuda zao si za mambo ya leo, ni mambo ya zamani hawana habari za mahali walipo sasa kiimani wao wana habari za mahali walipokuwa na walipo anzia kiimani.

Mtu wa nne na wa mwisho ninayemuandikia ujumbe huu ni yule ambaye bado si mwamini, bado hajampokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake.Kitabu hiki kina mambo ambayo yatamfanya mtu huyu aelewe hatari zinazomkabili na hasara anazozipata kwa kuwa katika kundi hili.

Ashukuriwe Mungu kwa sababu watu wengi duniani kote wanaendelea kuukubali wokovu na kuuamini, kanisa la Mungu linaendelea kukua na kuongezeka kama ilivyotabiriwa tangu mwanzo. Injili inaendelea kuhubiriwa na kuenezwa duniani kote huku ikidhaminiwa na kufadhiliwa na Yesu Kristo mwenyewe.

Pamoja na uzuri na uthamani wa wokovu, waamini wengine wamekuwa wakirudi nyuma na wengine hata kuacha kabisa imani hii iliyo ya thamani na bora.

Tutaona kwa upana wake kwa kadiri tutakavyokuwa tunaendelea mbele lakini kurudi nyuma katika wokovu kuna maana pana,zaidi ni ile hali ya mwamini kudumaa kiroho, kuuzoea wokovu na maonyo ya Mungu, kupungua na kuacha kuzaa matunda yatokanayo na wokovu. Ni kupungua na kuacha kufuata kanuni, itifaki na mfumo wa maisha ya imani.

Kumbuka kuwa, maisha ya wokovu ni mfumo kamili wa maisha wenye kujitegemea kikanuni, kiitifaki, kisheria na hata kimuundo.

***Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; (Waefeso 4:1*)**

Anavyosema muenende kama inavyoustahili wito wenu, kwa tafsiri nyingine ni kama anasema muishi kama wito wenu unavyotaka, kama inavyostahili mfumo na itifaki za maisha sawasawa na imani yenu

Kuacha wokovu ni ile hali au hatua ya mwamini kupoteza kabisa sifa na vigezo vya yeye kuitwa mwamini. Ni hatua ambayo mwamini anaondoka kabisa katika imani na kupoteza kabisa tabia za ki-Mungu ndani ya maisha yake. Hii ni ile hali ambayo kama wokovu ni klabu basi mwamini anapoteza sifa kabisa za kuwa mwanachama wa klabu husika.

Waamini wengine wamekuwa wakirudi nyuma na hata kuacha kabisa wokovu, bila kujua hatari na hasara zake katika maisha yao ya leo na kesho.

Ni kusudi la Mungu na lengo la kitabu hiki kukupa maarifa na miongozo kadhaa itakayokusaidia kukwepa hatari ya kutokuwa mwamini na hasara za kupoteza thamani ya imani hii. Mungu hapendi tupate hasara na wala hafurahii kamwe mwamini anaporudi nyuma na kuacha wokovu.

Ni maombi yangu kwa Mungu pia kuwa baada ya kusoma kitabu hiki, hali yako ya kiroho itaimarika zaidi, kwa wewe kuchukua hatua za kukwepa hatari na hasara za kurudi nyuma, kupoa na kuacha wokovu.